# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**JARIDA**

## Yaliyojiri mwezi NOVEMBA 2020





# Yaliyomo


1. Serikali yajipanga kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini.......................... 1
2. Wafugaji washauriwa kuwekeza katika Kilimo cha Malisho................ 3
3. Mifugo bora kuondoa umasikini kwa Wafugaji................................... 5
4. Dkt. Tamatamah aridhishwa na matokeo chanya ya Mradi wa Swiofish.......................................................................................... 6
5. Wafugaji wakijengewa uwezo watakuza uchumi wa Taifa.................. 8
6. Wafugaji na Wakulima kunufaika kupitia kiwanda cha Nyama Nguru Hills.......................................................................................... 9
7. Maabara ya kisasa ya utafiti Sekta ya Uvuvi yajengwa...................... 10
8. Serikali yapiga marufuku kulisha Mifugo vyakula vibovu.................... 12
9. Baraza la Veterinari lakifungia kituo cha Afya Sendeu....................... 13
10. Prof. Ole Gabriel awafunda wasomi Hombolo................................... 14
11. Serikali kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu.......................................... 15
12. Serikali yatumia Sh. Milioni 900 kukarabati Mabwawa mawili ya kunyweshea Mifugo.................................................................. 17
13. Utayari wa Wafugaji kushirikishwa kwenye mradi hufanya miradi yao kudumu......................................................................... 20
14. Watumishi watakiwa kulitunza basi jipya la Wizara............................ 22
15. Mradi wa Swiofish washirikisha wananchi kulinda Rasilimali za Uvuvi nchini......................................................................... 24

# SERIKALI YAJIPANGA KUIMARISHA SEKTA YA UVUVI NCHINI

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika mchakato wa kukamilisha Mpango kabambe wa miaka 15 ijayo kuanzia 2021 utakaosimamia sekta ya Uvuvi na kutoa dira ya kulinda rasilimali za uvuvi ili sekta hiyo iweze kutoa mchango mkubwa na endelevu katika pato la taifa.

Hilo limefahamika wakati Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi(Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah akifungua Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele yanayopaswa kuingizwa katika Mpango huo Kabambe unaofanyika Mkoani Singida Novemba 26-28, 2020.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa lengo la Serikali ni kuona sekta ya Uvuvi inaendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa zaidi ya ilivyosasa na ndio maana inaanda Mpango huo ili usimamizi wa rasilimali za uvuvi uwe imara.

“Ni mategemeo yetu kuwa mpango huu utatoa hamasa kwa sekta ya uvuvi katika kulinda usalama wa chakula kuanzia ngazi ya kaya na taifa, vilevile tunatarajia utuingize katika uchumi wa viwanda na uchumi wa bluu,” alisema Dkt.Tamatamah

Alisema kuwa pamoja na juhudu za Wizara za kusimamia maendeleo ya Sekta ya Uvuvi nchini, Sekta hiyo imeendele kukabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa ujumla zimekuwa zikiathiri ukuaji na uendelevu wa sekta hiyo.

Aliendelea kueleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imekuwa ikitekeleza mipango, mikakati na programu mbalimbali zinazolenga kuendeleza sekta ya uvuvi nchini, miongoni mwa mipango hiyo ni Mpango huo Kabambe wa Uvuvi unaotarajiwa kuanza kutumika mwaka 2021.

Mratibu wa Masuala ya Uvuvi kutoka Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ambao wanafadhili maandalizi ya mpango huo, Dkt. Oliver Mkumbo alisema shirika hilo limeamua kufadhili mpango huo ikiwa ni sehemu ya malengo yao ya kuhakikisha dunia inaondokana na njaa, umasikini na kuimarisha usalama wa chakula ili ifikapo mwaka 2030 pasiwepo na mtu atakayekuwa na njaa.

Aidha, wadau wa Sekta ya Uvuvi hawakusita kuonesha matumaini yao na mpango huo huku wakisema kuwa ukikamilika utajibu changamoto nyingi ambazo zimeendelea kukabili sekta hiyo.

Kiongozi wa Wavuvi Mkoani Kigoma, Francis John alisema kuwa mpango huo ambao utasimamia rasilimali za uvuvi utawasaidia kuimarisha biashara yao ya dagaa kutoka ziwa Tanganyika kwani mpango huo utawahakikishia uwepo wa dagaa wengi ambapo



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah akifungua Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele ya Mpango Kabambe unaofanyika Mkoani Singida Novemba 26-28, 2020.**

wataweza kuwa na mzigo wa uhakika wa kusafirisha kwenda kuuza dagaa wao katika nchi za Marekani, Astralia, Kanada, Uingereza na Denmark.

Naye, Raphael John, mdau wa sekta hiyo ya Uvuvi alisema kuwa  moja ya mambo yatayokwenda kuimarishwa kupitia mpango huo ni ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji jambo ambalo anasema litasaidia kupunguza utegemezi wa kupata mazao ya uvuvi kutoka maji ya asili pekee.

"Katika nchi nyingi zilizoendelea, ufugaji na ukuzaji wa viumbe maji umepewa kipaumbele sana, ni muhimu kuimarisha eneo hilo ili tusitegemee tu uvuvi wa mazao ya samaki katika maji ya asili, ni lazima tuanze sasa kabla rasilimali za asili katika bahari, mito na maziwa hazijaisha," alisema John

Mpaka sasa sekta ya uvuvi inachangia asilimia 1.7 katika pato la Taifa huku ikielezwa kuwa sekta hiyo inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wananchi takriban 202,000 na wananchi wengine wasiopungua Milioni 4.5 wamaendelea kutegemea kupata kipato chao kupitia sekta hiyo.

Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) limetoa Dola za Kimarekani 195,000 kwa ajili ya kufanya mapitio na kuandaa Mpango huo Kabambe wa sekta ya uvuvi ili sekta hiyo iweze kusimamiwa vizuri na kuendelea kuleta maendeleo yenye tija nchini.

Uandaaji wa mpango huo ni sehemu ya mipango mingi ambayo serikali imekusudia kuitekeleza, wakati akifungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Novemba 13, 2020 jijini Dodoma, Mhe. Rais, Dkt. John Joseph Magufuli alieleza mipango kadhaa ya kuboresha sekta ya uvuvi ikiwemo ununuzi wa meli nane (8), ujenzi wa Bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira elfu thelathini (30,000).



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (katikati-waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wadau wa Sekta ya Uvuvi walioshiriki Mkutano wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele ya Mpango Kabambe unaofanyika Mkoani Singida Novemba 26-28, 2020.**



**Sehemu ya Wadau wa Sekta ya Uvuvi wakiwa makini kufuatilia matukio katika Mkutano wa kupitia, kujadili na kuidhinisha masuala ya kipaumbele ya Mpango Kabambe unaofanyika Mkoani Singida Novemba 26-28, 2020.**

# WAFUGAJI WASHAURIWA KUWEKEZA KATIKA KILIMO CHA MALISHO

Wafugaji wa Ng'ombe wameshauriwa kujikita katika kilimo cha Malisho ili wawe na uhakika wa malisho bora kwa ajili ya mifugo yao na kuachana na uchungaji wa kutafuta malisho.

Mtendaji Mkuu wa Shamba la Ndoto, Hartmut Rottcher aliyasema hayo kwa Wakurugenzi na Mameneja wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi waliotembelea shamba la mfano la Ndoto lililopo Mkoani Iringa Novemba 27, 2020.

Rottcher alisema kilimo cha malisho yaliyo bora kinasaidia kuwapatia mifugo uhakika wa chakula bora huku akieleza kuwa mifugo ni muhimu kupewa pumba kwa kiasi na sio kuzidisha kwani kufanya hivyo hupelekea ng'ombe kupata asidi tumboni na kuuwa bakteria ambao husaidia kukata kata majani tumboni kwa mnyama.

Alisema kuwa yeye anafanya kilimo cha malisho kwa kumwagilia na ametenga maeneo katika mashamba yake illi kusaidia kulisha mifugo kwa mzunguko na kuipatia mifugo mahitaji wanayotaka na sio kuletewa chakula kwenye maboma yao.

"Njia ya kulisha kwa mzunguko husaidia kupata muda wa kuondoa magugu na kufanya shamba kuwa safi na malisho kustawi vizuri kwa wakati na linakuwa na rutuba ya kutosha," alisema Rottcher

"Kulisha chakula cha kutosha na cha aina tofauti husaidia mnyama kupata virutubisho vingi vinavyosaidia kujenga afya ya mifugo," Aliongeza Rottcher

Aidha, aliwashauri Wakurugenzi na Mameneja wa mashamba ya Serikali kutoa mifugo kwenda kujitafutia chakula na sio kuwaletea katika maboma yao kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia mifugo kupata kile wanachotaka na sio kuwapimia chakula jambo ambalo litawezesha kupata mifugo iliyo bora yenye nyama nyingi na maziwa ya kutosha yenye viwango.

Akieleza kuhusu ziara yao katika Shamba hilo, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ugani Dkt. Kejeri Gillah alisema lengo ni kujifunza na kubadilishana uzoefu katika kuboresha kosaafu na utunzaji wa mifugo, ustawishaji wa malisho bora kwa mifugo ya aina mbalimbali na namna ya uhifadhi wa malisho kwa matumizi ya kipindi cha kiangazi.



**Mtendaji Mkuu wa shamba la Ndoto Mkoani Iringa, Bw. Hartmut Rottcher, akielezea aina ya nyasi za malisho zilizopo shambani hapo na namna anafanya kilimo cha malisho ya Mifugo kwa watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi leo Novemba 27.2020 Mkoani Iringa.**

“Ni mategemeo yetu kwamba safari hii itakuwa ya mafanikio makubwa sana kwetu na tutaweza kuboresha mifugo yetu na kustawisha malisho ya mifugo kama tutafuata yale yote tutakayoelekezawa” alisema Dkt. Gillah

Ziara hiyo iliratibiwa na Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ugani, Dkt. Kejeri Gillah.

Wengine walishiriki katika ziara hiyo ni Mameneja kutoka Shamba la kitulo, Sao hill, Langwira, Vikuge, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Uyole na meneja wa Ranchi ya Kalambo.



**Kaimu Mkurugenzi Ugani Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Kejeri Gillah akieleza lengo la safari yao ya mafunzo ya kutembelea shamba la Ndoto ikiwa ni pamoja na kubadilisha uzoefu katika uboreshaji wa kosaafu na utunzaji Mifugo, uhifadhi wa malisho bora, udhibiti wa magonjwa na matumizi ya madawa shambani leo Novemba 27. 2020 kwenye shamba la Ndoto Mkoani Iringa.**



**Watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakimsikiliza kwa makini Mtendaji Mkuu wa Shamba la Miombo Bw. Rex Fey ( kushoto) wakati akiwasilisha mada ya mbegu, malisho na namna bora ya kulisha mifugo kwenye Shamba la Ndoto Mkoani Iringa ( 27/11/2020)**

# MIFUGO BORA KUONDOA UMASIKINI KWA WAFUGAJI

Wafugaji nchini wametakiwa kufuga mifugo bora itakayowasaidia kuondokana na umasikini na kuchangia ukuaji wa pato la taifa.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa zoezi la uhimilishaji wa ng'ombe lililofanyika wilayani Musoma, Mkoa wa Mara Novemba 25, 2020.

Prof. Gabriel alisema kuwa utajiri unaotokana na mifugo hauletwi kwa wingi wa mifugo inayomilikiwa na mfugaji bali utajiri huletwa kutokana na ubora wa mifugo aliyonayo mfugaji. Hivyo amewasihi wafugaji kuhakikisha wanatumia njia ya uhimilishaji ili kuboresha kosaafu.

"Ng'ombe walioboreshwa kosaafu zao huweza kutoa zaidi ya lita arobaini (40) za maziwa kwa siku tofauti na ngombe wa asili ambao huishia kutoa lita mbili mpaka nne (4) kwa siku, hivyo kupitia maziwa peke yake mfugaji anaweza kuimarisha kipato chake na pato la taifa kwa ujuml," alisema Prof. Gabriel.

"Dhana hii tunayoileta ya uhimilishaji ni kwamba tuwe na mifugo mingi lakini yote iwe bora kwani mifugo ni mtambo unaotembea kwani ng'ombe anakula majani lakini anakupatia maziwa meupe na nyama nyekundu," aliongeza Prof. Gabriel.

Prof. Gabriel amesema kuwa upandishaji wa ng'ombe kwa kutumia njia ya uhimilishaji una faida kubwa kwani mfugaji atapata mbegu/mbari nzuri (mfugaji ataboresha aina ya ng'ombe atakayezaliwa), pili mfugaji ataboresha mazao ya mifugo kutokana na uhimilishaji na pia ataepusha usambazaji wa magonjwa kutoka kwa dume kwenda kwa jike.

Wizara imeshaweka mpango ambapo katika maeneo yote ambayo zoezi la uhimilishaji litazinduliwa, ng'ombe 1000 wa kwanza watahimilishwa bure kwa gharama za wizara. Lakini pia wizara itagharamia gharama



**Pichani ni zoezi la upandikizaji wa mimba kwa njia ya mrija (Uhimilishaji) kwa Ng'ombe.**

za usafirishaji wa mbegu mpaka kwenye makao makuu ya mikoa lengo ni kurahisisha upatikanaji.

Katibu Mkuu Gabriel amesema wizara imejipanga vizuri kutekeleza maelekezo ya Rais Magufuli katika kuhakikisha sekta inakua kwenda kwenye uchumi wa viwanda, na kuendelea kupanda katika uchumi wa kati kiwango cha juu. Sekta ya mifugo kwa sasa inachangia asilimia 7.64 katika pato la taifa na inakua kwa asilimia 5 kwa mwaka.

"Niwaombe wafugaji kote nchini kuwa na mwitikio mzuri katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali, kwani ni rahisi kumlazimisha ng'ombe kwenda mtoni lakini si rahisi kumlazimisha ng'ombe kunywa maji, hivyo wafugaji changamkieni fursa hii ya uhimilishaji ili mboresha kosaafu za mifugo yenu na mkifanya hivyo mtakuwa mmeitendea haki nia njema ya serikali ya kubadilisha Maisha ya wafugaji," alisema Prof. Gabriel.

Vilevile amewaomba viongozi katika ngazi za mikoa, wilaya na halmashauri kuhakikisha wanasimamia na kufuatilia masuala ya mifugo katika maeneo yao ili ufugaji uweze kuleta tija kwa wafugaji na kuchangia katika pato la taifa.

Ng'wenda Maswi ambaye ni mfugaji amesema fursa hii ya uhimilishaji ni nzuri sana kwani inawasaidia kupata ng'ombe ambao wataweza kutoa maziwa mengi tofauti na ng'ombe wa asili. Vilevile amempongeza Katibu Mkuu Gabriel kwa kazi nzuri ya kuwafikia wafugaji na kuwapelekea huduma hiyo. Pia amewasihi wafugaji wenzake kuhakikisha wanaitumia fursa hiyo waliyoipata yenye lengo la kuboresha kosaafu za mifugo yao na kuendelea kusikiliza ushauri kutoka kwa wataalam.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dkt. Vicent Naano amewasihi wafugaji kujenga tabia ya kuwasikiliza wataalam wa mifugo ili waweze kupata ushauri sahihi utakaowasaidia kuboresha mifugo yao na kuwanyanyua kiuchumi.

# DKT. TAMATAMAH ARIDHISHWA NA MATOKEO CHANYA YA MRADI WA SWIOFish

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah amefanya ziara ya kikazi ya siku mbili katika mikoa ya Pwani na Tanga na kubainisha kuridhishwa na ujenzi wa majengo maalum kwa ajili ya ofisi za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish).

Akizungumza na viongozi wa BMU na wananchi kwa nyakati tofauti katikati ya mwezi Novemba, 2020, mara baada ya kutembelea majengo hayo kwenye Kata ya Dunda Wilaya ya Bagamoyo na Kata ya Saadani Wilaya ya Chalinze katika Mkoa wa Pwani, Kata ya Kipumbwi Wilaya ya Pangani na Kata ya Zingibari Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, Dkt. Tamatamah alisema ujenzi wa majengo hayo unaendelea vizuri huku akiwataka makandarasi kuhakikisha majengo hayo yanakamilika ifikapo mwezi Desemba Mwaka 2020 kama makubaliano yalivyo kwenye mikataba.

“Nimeridhishwa na ujenzi wa baadhi ya majengo hayo kupitia mradi wa SWIOFish ila ninawaagiza makandarasi kuhakikisha majengo haya yanakamilika kwa wakati ili kuanzia Mwezi Januari Mwaka 2021 yaanze kutumika na viongozi wa BMU kama ofisi katika shughuli mbalimbali za kulinda rasilimali za uvuvi kwenye Ukanda wa Pwani, mkandarasi yeyote ambaye hatakamilisha jengo kwa wakati tutamchukulia hatua.” Amefafanua Dkt. Tamatamah

Aliongeza kuwa mradi huo ambao unahusisha majengo matano ya BMU likiwemo la Kata ya Sudi Wilaya ya Mtama Mkoani Lindi utakaogharimu zaidi ya Shilingi Milioni 700 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, kukamilika kwake kutasaidia kusimamia zaidi rasilimali za uvuvi ikiwa ni pamoja na kutunza nyaraka muhimu.

“BMU zina matatizo ya ofisi na mmekuwa mkishiriki kutokomeza uvuvi haramu, mkikamata nyavu haramu mnaziweka wapi? Ndiyo maana tunawajengea ofisi kupitia mradi wa SWIOFish. Nia ni ulinzi shirikishi kwa kuwapatia zana, elimu na miundombinu mbalimbali.” Amebainisha Dkt. Tamatamah

Aidha, alisema mara baada makandarasi kukabidhiwa ramani za majengo hayo Mwezi Julai Mwaka 2020 na kutakiwa kuanza mara moja ujenzi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayosimamia mradi wa SWIOFish kwa upande wa Tanzania Bara inatarajia mara baada ya kukabidhiwa majengo hayo Mwezi Desemba Mwaka 2020, mradi utanunua pia samani na vitendea kazi vingine vya ofisi zikiwemo kompyuta.

Pia, alisema lengo la mradi huo unaotekelezwa katika nchi tatu za Tanzania, Msumbiji na Comoro kwa Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ni kuwajengea uwezo wananchi hususan jamii ya wavuvi kusimamia



**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga Bw. Oscar Mbenje akimueleza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah namna halmashauri hiyo ilivyofanikiwa kukusanya mapato mengi kupitia Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU).**

rasilimali za uvuvi kupitia vikundi, ambapo kwa Zanzibar unasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hali kadhalika ikiwemo taasisi ya muungano ya Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (DFSA).

Katika ziara hiyo ya kikazi ya siku mbili kwenye mradi wa ujenzi wa majengo ya ofisi za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah amesema mradi huo wa miaka sita ulioanza Mwezi Juni Mwaka 2015 na kutarajiwa kukamilika Mwezi Mei Mwaka 2021, umekuwa ukiendeleza jitihada za serikali ambazo imekuwa ikifanya tangu zamani kwenye maeneo yenye shughuli za uvuvi kote nchini katika kusimamia rasilimali za uvuvi ili kutoa ajira na kuhakikisha mazao ya uvuvi yananufaisha taifa na mwananchi mmoja mmoja.

“Tunatarajia mradi huu kukamilika Mwezi Mei Mwaka 2021 ni mategemeo yetu Benki ya Dunia itaendelea kutupatia mradi huu ambao umekuwa na matokeo chanya katika kulinda rasilimali za uvuvi, pia maeneo ambayo mradi huu bado haujafika nchini, serikali imekuwa ikitenga fedha kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinalindwa kwa kukomesha uvuvi haramu na kutoa elimu juu ya mchango wa seta ya uvuvi kwa jamii ya wavuvi nchini. Amesema Dkt. Tamatamah

Ili kuhakikisha serikali inakusanya mapato mengi kupitia sekta ya uvuvi katibu mkuu huyo amewataka viongozi wa halmashauri nchini kwenye maeneo zilipo shughuli za uvuvi kuvipatia vikundi vya BMU mamlaka ya kukusanya mapato, akibainisha kuwa baadhi ya halmashauri ambazo zimefanya hivyo zimekuwa zikipatiwa makusanyo mengi tofauti na yale ambayo wamekuwa wakikusanya siku za nyuma.

Nao baadhi ya viongozi wa BMU wa maeneo ambayo majengo hayo yanajengwa wamepongeza juhudi za serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kubainisha kuwa mara baada ya kukamilika kwa majengo hayo na hatimaye kukabidhiwa kwa ajili ya ofisi watahakikisha wanayatumia kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kuyatunza ili yadumu kwa muda mrefu.

Wamebainisha kitendo cha kujengewa majengo maalum kwa ajili ya ofisi kuna dhihirisha namna serikali inavyotambua mchango wa BMU katika kuhakikisha wanaisaidia kulinda rasilimali za uvuvi.

Aidha Dkt. Tamatamah amepata pia fursa ya kufika na kukagua nyumba za Taasisi ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kwenye Hifadhi ya Silikanti Tanga zilizopo Kata ya Kigombe Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga, ambazo pia zimejengwa kupitia mradi wa SWIOFish kwa ajili ya watumishi wa hifadhi hiyo na kuridhishwa na nyumba hizo ambazo tayari zimekabidhiwa wizarani tangu Mwezi Februari Mwaka 2020 na kutaka watumishi watakaotumia nyumba hizo kuzitunza ili ziwe na tija kwao.

Katika ziara hiyo Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah amezungumza na jamii ya wavuvi na kusikiliza baadhi ya changamoto zinazowakabili na kuwaahidi kuzifanyia kazi na kwamba wizara imekuwa ikifanya marekebisho ya kanuni na tozo mbalimbali za uvuvi pamoja na kuhakikisha wavuvi wanapata masoko ya mazao yao.

Pia, aliwasisitiza akinamama kuendelea na kilimo cha mwani ambacho kimekuwa na tija kwao katika kuendesha familia zao.



**Mratibu wa Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) Bw. Nichrous Mlalila (wa kwanza kulia) akimuelezea Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah (wa pili kutoka kushoto), namna mkandarasi anayejenga jengo la BMU Kata ya Saadani anavyochelewesha ujenzi huo, hali iliyomlazimu Dkt. Tamatamah kumtaka mkandarasi huyo kukamilisha ujenzi kwa mujibu wa mkataba.**

# WAFUGAJI WAKIJENGEWA UWEZO WATAKUZA UCHUMI WA TAIFA- MONGELA.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongela amesifu juhudi zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kuhakikisha wafugaji wake wanafanya shughuli hiyo kwa tija na kwa kuzingatia dhana ya ukuzaji wa uchumi wao.

Mhe. Mongela aliyasema hayo leo (12.11.2020) baada ya kupokea timu ya wataalam wa Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo (Wizara ya Mifugo na Uvuvi) ambao wamefika mkoani humo kwa ajili ya kutoa mafunzo ya siku mbili kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo kuhusu ukaguzi wa maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo

“Tunajitahidi sana kukuza tasnia ya ufugaji lakini uwepo mafunzo kama haya unawafanya wafugaji wetu wasiishie tu kufuga bali wafuge kwa tija na kukuza uchumi wao” amesema Mhe. Mongela.

Mhe. Mongela aliishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea na jitihada hizo za kujenga uwezo kwa wafugaji ili kuwafanya kuwa wafugaji bora wenye uelewa na ujuzi wa ufugaji wa kisasa badala ya ufugaji wa asili ambao haukuwa na tija kwa mfugaji pamoja na kuwa na idadi kubwa ya mifugo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo Dkt. Asimwe Rwiguza amesema kuwa wakaguzi hao ni sehemu ya wakaguzi 129 walioteuliwa kutoka kwenye Halmashauri na Sekretarieti za mikoa hapa nchini ambao baada ya kupatiwa mafunzo hayo watawawezesha wafugaji waliopo kwenye maeneo yao elimu kuhusu chakula bora cha mifugo ili waweze kuiboresha na kuongeza tija zaidi kwenye tasnia hiyo.

“Semina hii ni muhimu sana hivyo ninaomba tushirikiane na kwa sababu ninafahamu kuwa wote mna ujuzi hivyo leo tupo hapa kwa



**Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo Dkt. Asimwe Rwiguza (Kulia) akimueleza Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongela (kushoto) kuhusu Mafunzo ya ukaguzi wa maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo yaliyofanyika leo (12.11.2020) na kutarajia kuhitimishwa kesho mkoani humo. Katikati ni Katibu Tawala wa Mkoa huo Ndg. Emanuel Tutuba.**



**Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongela (katikati) akifafanua juu ya namna mkoa huo unavyozipa kipaumbele sekta za Mifugo na Uvuvi mbele ya timu ya wataalam wa Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi waliofika Ofisini kwake mapema leo (12.11.2020) muda mfupi kabla ya kuanza mafunzo kwa wakaguzi wa Vyakula vya Mifugo kutoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida na Arusha yaliyofanyika leo na kuendelea kesho mkoani humo**

ajili ya kuongezeana uwezo wa kuwahudumia vizuri wafugaji wetu hasa ikizingatiwa kuwa takribani asilimia 70 ya mahitaji ya mfugo ni chakula” Ameongeza Dkt. Rwiguza

Mafunzo hayo yaliyofunguliwa na Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza Bw. Emmanuel ni ya awamu ya pili ambapo awamu ya kwanza ilifanyika mkoani Morogoro na kuhusisha Mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga na Dodoma.

# WAFUGAJI NA WAKULIMA KUNUFAIKA KUPITIA KIWANDA CHA NYAMA NGURU HILLS

Serikali imesema katika kuboresha na kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini ukiwemo Mkoa wa Morogoro, inasisitiza uwepo wa miradi ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwa makundi yote mawili.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel alisema hayo katika Wilaya ya Mvomero Mkoani Morogoro Novemba 29, 2020 alipotembelea ujenzi wa mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills na kubainisha kuwa mradi huo unaotarajia kukamilika mwezi Aprili Mwaka 2021 utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji na wakazi wa Mkoa wa Morogoro.

"Tumekuja kuangalia shughuli zinazoendelea kutokana na kikao ambacho tulikuwa nacho katika ofisi ya katibu tawala wa mkoa na mkuu wa Mkoa wa Morogoro katika kuboresha shughuli za mifugo kwenye mkoa huo na kuondoa changamoto za migogoro ya wafugaji ambapo uongozi wa mkoa waliniambia juu ya mradi huu ambao utakuwa na msaada mkubwa sana kwa wakulima na wafugaji wa mkoa wa Morogoro na nchi kwa ujumla." Amesema Prof. Gabriel

Prof. Gabriel alibainisha kuwa mradi huo wa kipekee ambao mara baada ya kiwanda hicho kukamilika kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe zaidi ya 200 na mbuzi zaidi ya 1,000 kwa siku, kumejengwa mabwawa makubwa ambayo yatakuwa yanakusanya maji yanayotoka kwenye machinjio, kisha kutibiwa kabla ya kutumika tena kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

"Mradi huu una jambo mahsusi kuliko mingine, maji haya ya mabwawa yatatumika kwa ajili ya umwagiliaji huu ni moja kati ya miradi ambapo wafugaji na wakulima watanufaika ili wote waone huu mradi ni wa kwao kwa ajili ya uchumi wetu." Ameongeza Prof. Gabriel

Aidha, alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 25, ambao unashirikisha wabia mbalimbali ukiwemo Mfuko wa Pesheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ni azma ya serikali katika kuzidi kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini kwenye sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Mifugo hivyo kuwataka wafugaji kuboresha mifugo yao kwa kufuga ng'ombe bora wa kisasa na kupitia miradi ya kunenepesha mifugo ili waweze kuuza mifugo yenye ubora katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo hapa nchini ili sekta izidi kukua na kuchangia pato la taifa kupitia uchumi wa viwanda.



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel (wa kwanza kushoto) akizungumza na baadhi ya viongozi wa Ranchi ya Nguru Hills juu ya mradi wa kiwanda cha nyama kinachojengwa katika ranchi hiyo huku akiwataka wahakikishe mara baada ya kiwanda hicho kitakapoanza kufanya kazi, kitoe bidhaa bora ili kushindana na soko la kimataifa. Meneja Mkuu wa ranchi hiyo Bw. Paul Phillips (aliyesimama katikati) amemuhakikishia katibu mkuu huyo kuzingatia maelekezo yake**

Pia, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha Tanzania inakuwa na mifugo mingi na bora kwa kuhakikisha mifugo inaogeshwa ili kujikinga dhidi ya magonjwa na kuwataka wakurugenzi wa halmashauri kote nchini, kuhakikisha maeneo yao yana majosho ya kutosha kwa ajili ya kuogeshea mifugo na kuwataka wayafanyie ukarabati majosho ambayo hayafanyi kazi.

"Tufuge kisasa Namibia, Botswana wana ng'ombe wachache lakini wanauza kwa wingi nyama nje ya nchi, ndiyo maana tunaimarisha afya za mifugo, ndiyo maana nchi nzima tunashughulika na masuala ya uogeshaji niwatake wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe kwenye maeneo yao kuna majosho ya kutosha na niwatake yale ambayo hayafanyi kazi vizuri yaboreshwe," aliongeza Prof. Gabriel

Aidha, amelitaka pia Dawati la Sekta Binafsi lililo chini ya wizara hiyo pamoja na Idara ya Uzalishaji na Masoko kwa kushirikiana na PSSSF kukutana haraka ili kujadili changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika mradi wa kiwanda cha nyama Nguru Hills ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero Bw. Hassan Chama Hassan amemwambia katibu mkuu huyo kuwa, mradi huo ukikamilika kwa wakati wafugaji watanufaika kwa kuwa wanakabiliana na changamoto ya kuuza mifugo yao kupitia minada ambapo wanakutana na madalali ambao wanafanya bei za mifugo kuwa chini, huku Meneja Ujenzi wa mradi huo kutoka PSSSF Mhandisi Grayson Bambaza akibainisha kuwa wafugaji watakuwa wanauza mifugo yao kwa kilo na siyo kwa kukadiria kulingana na umbo la mfugo.

Mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills unaotarajia kukamilika mwezi Aprili Mwaka 2021, unategemewa kutoa ajira kwa wafanyakazi 120 hadi 200 kulingana na uzalishaji.

# MAABARA YA KISASA YA UTAFITI SEKTA YA UVUVI YAJENGWA

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah amesema serikali imetilia mkazo suala la utafiti katika sekta ya uvuvi nchini ili kuhakikisha inapata taarifa sahihi ya maeneo ya mavuvi, kuzalisha vifaranga bora vya samaki pamoja na chakula bora cha samaki.

Akizungumza jijini Dar es Salaam Novemba 18, 2020 wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya utafiti wa uvuvi itakayotumika na Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) inayojengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), Dkt. Tamatamah alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wa masharti nafuu wa Shilingi Bilioni 2.6 unalenga kukuza sekta ya uvuvi nchini.

“Kwenye uchumi wa bluu katika awamu hii tunategemea meli nane kwenye uvuvi wa bahari kuu hivyo unapofanya uvuvi wa bahari kuu haujiendei tu lazima watafiti kama TAFIRI waende baharini wajue chambo wanapata wapi kwa ajili ya kuvua samaki, pia tuna mpango wa kuongeza uzalishaji wa samaki kupitia ufugaji kwenye maeneo mawili ya chakula bora pamoja na vifaranga bora hivyo tafiti ni muhimu kupitia maabara hii.” alisema Dkt. Tamatamah

Aliongeza kuwa katika miaka mitano ijayo serikali itapunguza au kuondoa kabisa changamoto ya upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki na chakula bora cha samaki kutokana na watu wengi kujitokeza katika ufugaji wa samaki ambapo mahitaji ni vifaranga milioni 50 kwa mwaka lakini kwa sasa vifaranga vinavyozalishwa hapa nchini ni milioni 30 pekee.



**Muonekano wa ujenzi wa jengo la maabara ya uvuvi litakalotumika na Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) linalojengwa kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), jijini Dar es Salaam.**



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah (katika) akiongozwa na Mratibu wa Mradi wa SWIOFish Bw. Nichrous Mlalila (Kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Dkt. Ismael Kimirei kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la maabara linalotakiwa kukabidhiwa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi tarehe nane mwezi Desemba 2020.**

Kwa upande wake mratibu wa mradi wa SWIOFish Tanzania Bara Bw. Nichrous Mlalila alisema baada ya kukamilika kwa jengo hilo wataalamu watajikita katika kufanya utafiti ambapo kwa sasa sampuli za mazao ya samaki zimekuwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi kwa ajili ya tafiti hali ambayo inahatarisha usalama wa nchi na rasilimali zake.

Aidha, alisema serikali inatarajia kujenga maabara nyingine kupitia mradi huo kwa ajili ya kuzalisha vifaranga bora vya samaki wa baharini pamoja na mbegu za zao la mwani katika kukuza sekta ya uvuvi hapa nchini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Dkt. Ismael Kimirei alisema taasisi hiyo ina mikakati mingi katika kukuza tafiti za uvuvi hapa nchini kwa kutumia teknolojia ya kisasa pamoja na kupunguza gharama za kutuma sampuli za uvuvi kwenda nchi za nje na hivyo sampuli zote kufanyiwa kazi katika maabara hiyo.

Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umeanza kazi hapa nchini mwezi Juni mwaka 2015 na unatarajia kukamilika mwezi Mei mwaka 2021, huku serikali ikiwa na matumaini makubwa ya mradi huo kuendelea kuwepo hapa nchini kutokana na matokeo chanya katika kukuza sekta ya uvuvi kupitia mradi huo, ambapo ujenzi wa maabara hiyo unatarajia kuwa umekamilika na kukabidhiwa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi tarehe 8 mwezi Desemba mwaka 2020.

# SERIKALI YAPIGA MARUFUKU KULISHA MIFUGO VYAKULA VIBOVU

Serikali imepiga marufuku matumizi ya vyakula vilivyopoteza ubora wa kutumiwa na binadamu na kutumiwa kama vyakula vya mifugo kabla ya kuthibitishwa kwanza na wataalam wa maabara ya mifugo.


Hayo yalisemwa leo (13.11.2020) na Mkurugenzi wa Uendelezaji Malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo Dkt. Asimwe Rwiguza ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha mafunzo ya siku mbili ya wakaguzi wa vyakula vya mifugo kutoka mikoa ya Mwanza,Shinyanga, Singida na yaliyofanyika Mkoani Mwanza.

“Kumekuwa na mazoea ya vyakula ambavyo vimeshapoteza ubora wa matumizi ya binadamu kutumika kama vyakula vya mifugo hivyo ninapenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wafugaji, wazalishaji na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na uzalishaji wa vyakula vya binadamu kuwa ni marufuku kutumia vyakula hivyo bila Wizara yenye dhamana kuwa na taarifa na kujiridhisha kitaalam kama chakula hicho kinafaa au la” Amesisitiza Dkt. Rwiguza.

Aidha Dkt. Rwiguza amebainisha madhara yanayoweza kumpata mtu ambaye atatumia mazao ya mfugo uliokula vyakula hivyo kuwa ni pamoja na kupatwa na magonjwa mbalimbali kama vile Kansa.


Upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji Malisho na rasilimali za vyakula vya Mifugo Bw. Roggers Shengoto amesema kuwa mafunzo hayo yamekuwa na manufaa makubwa kwa sababu sehemu zaidi ya asilimia 90 ya wataalam walioalikwa walishiriki.

“Pia kupitia mafunzo haya tumegundua kuwa bado kuna haja ya Halmashauri za vijiji kutenga maeneo ya malisho ya mifugo na pia wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo bado hawazingatii sheria na kanuni za kufanya shughuli hizo hivyo tuna imani wataalam hawa wataenda kuleta mabadiliko katika maeneo yote yenye changamoto kwa mfugaji” Ameongeza Shengoto.



**Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo (Wizara ya Mifugo na Uvuvi) Bw. Roggers Shengoto akiwasilisha mada ya sheria na kanuni za Maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo tarehe 12.11.2020 wakati wa mafunzo kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo yaliyofanyika Mkoani Mwanza kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu huo.**

**PICHA YA CHINI: Sehemu ya wakaguzi wa Vyakula vya Mifugo kutoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida na Arusha wakifuatilia kwa umakini mafunzo hayo.**



Nao baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo wamesema kuwa wamenufaika na yote waliyofundishwa ambapo wameahidi kuyafanyia kazi na kubadilisha utendaji wao pindi wakirejea kwenye vituo vyao vya kazi.

“Kwa mfano, zamani nilikuwa naenda kwa mdau kama Mkaguzi na nilikuwa natumia lugha ya mamlaka lakini kupitia mafunzo haya nimefundishwa kumfuata mdau kama rafiki na kuzungumza naye kwa lugha ya kawaida” Amesema mmoja wa washiriki Veronica Ngoso.

Takribani wakaguzi 129 nchi nzima wanatarajiwa kupatiwa mafunzo hayo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa kufuata taratibu, sheria na kanuni.

# BARAZA LA VETERINARI LAKIFUNGIA KITUO CHA AFYA SENDEU

Baraza la Veterinari Tanzania limekifungia kituo cha huduma ya afya ya wanyama cha Sendeu kilichopo Wilayani Longido, Mkoani Arusha kwa kubainika kutokuwa na wataalam waliosajiliwa na Baraza hilo.

Baraza lilifikia hatua hiyo mkoani humo Novemba 22, 2020 kufuatia ukaguzi unaoendelea kufanywa katika mikoa mbalimbali nchini na wakaguzi wa baraza hilo ikiwa ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku.

Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania, Dkt. Bedan Masuruli alieleza kuhusu uamuzi huo wa baraza ofisini kwake, jijini Dodoma Novemba 23, 2020.

Dkt. Masuruli alisema kuwa uamuzi huo wa baraza umefikiwa baada ya kujiridhisha kuwa kituo hicho cha afya ya wanyama kinaendesha shughuli zake kinyume cha taratibu.

Aliongeza kuwa wakaguzi wa baraza walipoenda kufanya ukaguzi katika kituo hicho walibaini mapungufu hayo ambayo kimsingi ni kinyume cha taratibu na ni hatari kwa afya ya wanyama.

Aidha, Dkt. Masuruli aliwahimiza wamiliki wote wa vituo vya afya ya mifugo kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinasimamiwa kikamilifu na huduma zinazotolewa na wataalam wa mifugo waliosajiliwa na baraza la veterinari Tanzania.

Dkt. Masuruli amevisisitiza vituo vingine vyote nchini kuzingatia taratibu zote za kutoa huduma, na baraza halitasita kuchukua hatua kwa vituo vyote vitakavyoshindwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utoaji huduma ya afya ya wanyama.

Awali msajili wa Baraza hilo alisema walifanya ukaguzi kwenye mikoa ya Tanga, Shinyanga, Simiyu na Ruvuma na kubaini changamoto za ukiukwaji wa maadili ya utoaji huduma ya afya ya wanyama na kupelekea kulipishwa faini na wengine kufungiwa kutoa huduma ya afya ya wanyama.




**Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania, Dkt. Bedan Masuruli akisisitiza jambo wakati alipokuwa akiongea na wamiliki wa vituo vya afya ofisini kwake Dodoma tarehe 23/11/2020.**

# PROF. OLE GABRIEL AWAFUNDA WASOMI HOMBOLO

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel amewaeleza wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa- Hombolo kuwa wao ni Viongozi watarajiwa hivyo wanawajibu wa kuhakikisha watakapokuwa viongozi wanakidhi matarajio ya wale watakaokuja kuwaongoza.

Prof. Gabriel aliyasema hayo wakati akiwasilisha mada iliyohusu nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii anayoiongoza kwenye hafla ya kuwatunuku zawadi wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao na wafanyakazi bora wa chuo cha Hombolo iliyofanyika katika chuo hicho kilichopo Dodoma Novemba 25, 2020.

Alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho nchi ya Tanzania imeingia katika uchumi wa kati viongozi wanawajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wanakidhi matarajio ya Watanzania.

Prof. Gabriel aliongeza kuwa nchi nyingi na taasisi zimekuwa zikikwama kufikia malengo tarajiwa kwa sababu ya kukosa usimamizi mzuri.

“Kuwa na rasilimali ni jambo moja, lakini kusimamia rasilimali hizo ni jambo la muhimu zaidi, taasisi nyingi zimekwama kwa kushindwa kusimamia rasilimali zake ikiwemo rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali miundombinu,” alisema Prof. Gabriel

Kwa mantiki hiyo aliupongeza Uongozi wa Chuo cha Hombolo kwa kusimamia agenda ya uongozi huku akisema kuwa elimu hiyo wanayoitoa kwa wanafunzi wa chuo hicho itawasaidia wanafunzi hapo mbeleni watakapokuwa viongozi.

Aliendelea kusema kuwa kiongozi yeyote wa kuchaguliwa au kuteuliwa ili awe kiongozi bora ni muhimu kuzingatia mambo matatu ambayo ni kufahamu hasa anaowaongoza wanamahitaji gani? pia Kiongozi atambue kuwa hatakumbukwa kwa cheo chake bali kwa mchango wake kwa jamii ile anayoiongoza na tatu, awe mtu anayewashirikisha wale anaowaongoza katika kutatua changamoto zao.

“Washirikishe wale unaowaongoza na ndipo utakapoweza kutatua changamoto, kiongozi mzuri ni yule anayeziona changamoto na kuzibadilisha kuwa fursa, na kwa kufanya hivyo ndipo utaweza kukidhi matarajio ya wale unaowaongoza,”alisisitiza Prof. Gabriel

Katika hafla hiyo ya kumi na mbili (12) ya chuo hicho, Prof. Elisante Ole Gabriel alikuwa Mtoa mada maalum na aliwasilisha mada hiyo ya nafasi ya viongozi wa kuchaguliwa na wakuteuliwa katika kuleta maendeleo kwa jamii ili kuwakumbusha wajibu wao mkubwa kwa jamii.



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (kulia) akifurahia jambo alipokuwa akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Elimu, Gereld Mweli (kushoto) walipokutana kwenye hafla ya kutunukiwa zawadi wafanyakazi na wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa- Hombolo waliofanya vizuri katika masomo yao. Prof. Elisante Ole Gabriel alikuwa Mtoa mada maalum katika hafla hiyo iliyofanyika katika chuo hicho kilichopo Dodoma Novemba 25, 2020.**



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel akiwasilisha mada katika hafla ya kutunukiwa zawadi Wafanyakazi na Wanafunzi waliofanya vizuri wa Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo iliyofanyika katika chuo hicho kilichopo Dodoma Novemba 25, 2020.**

# SERIKALI KUIMARISHA UVUVI WA BAHARI KUU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amesema kuwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo ya awamu yake ya pili ya uongozi atahakikisha sekta ya uvuvi inakuzwa ikiwemo kuimarisha shughuli za uvuvi wa bahari kuu kwa kununua Meli nane (8) zitakazofanya kazi katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ulioko Visiwani Zanzibar na Tanzania bara.

Dkt. Magufuli aliyasema hayo wakati akitoa hotuba yake ya kulifungua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma Novemba 13, 2020.

Wakati akilihutubia bunge hilo lililosheheni Wabunge wengi wapya, Dkt. Magufuli alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yanayofaa kwa shughuli za uvuvi ikiwemo Mito, Bahari na Maziwa hali ambayo inaifanya sekta ya uvuvi kuwa na nafasi kubwa ya kutoa mchango katika kukuza pato la taifa, kupambana na umasikini na tatizo la ajira.

Alisema pamoja na fursa hiyo iliyopo nchini bado mpaka sasa mchango wa sekta ya uvuvi upo chini hivyo serikali imekusudia kuweka nguvu zaidi ili kukuza sekta hiyo iweze kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

“Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2018 ya Kamati ya



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akihutubia pamoja na kulifungua rasmi Bunge la 12 jijini Dodoma Novemba 13, 2020.**

Bunge kuhusu shughuli za uvuvi wa bahari kuu, kama uvuvi wa bahari kuu utasimamiwa vizuri tunaweza kuiingizia serikali mapato ya moja kwa moja ya shilingi bilioni 352.1 kwa mwaka," alisema Dkt. Magufuli

Aliendelea kueleza kuwa kufuatia hali hiyo serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha inasimamia mfumo mzima ikiwemo udhibiti wa shughuli za uvuvi ili malighafi itayokuwa inapatikana iweze kuchakatwa hapa nchini kwa lengo la kukuza thamani ya mazao ya baharini.

"Kwa bahati nzuri tumetunga sheria mpya ya kuendeleza shughuli za uvuvi nchini hivyo itasaidia katika usimamizi wa shughuli za uvuvi," alieleza Dkt. Magufuli

Aliongeza kwa kusema kuwa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la kuendeleza Kilimo (IFAD), itanunua Meli nane (8) za uvuvi katika bahari kuu ambapo 4 zitakuwa zikifanya shughuli zake Visiwani Zanzibar na 4 nyingine zitafanya shughuli zake katika ukanda wa pwani wa bahari ya hindi upande Tanzania bara.

"Kama mnavyofahamu suala la uvuvi ni la Muungano, tunakusudia kujenga bandari kubwa ya uvuvi itakayotoa ajira elfu thelathini (30,000) na tutaendelea kuhamasisha sekta binafsi kujenga Viwanda vya kuchakata samaki, sambamba na hilo tutakuza shughuli kwenye maziwa yetu makuu yaani Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika," alisisitiza Dkt. Magufuli

Aidha, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya uongozi wake serikali itahamasisha wavuvi wadogo wadogo kujiunga katika vikundi ili waweze kuwapatia mitaji, vifaa, ujuzi na zana za uvuvi.

"Tutapitia upya tozo ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia uwekezaji kwa wavuvi wetu," alifafanua Dkt. Magufuli

Kuhusu ujenzi wa Mabwawa, Dkt. Magufuli alisema kuwa watahamasisha watu binafsi kujenga mabwawa na kufuga kisasa kwa kutumia vizimba huku akisisitiza kuwa sekta ya uvuvi ni lazima itoe mchango mkubwa katika uchumi wa nchi na hivyo kuwataka wateule wote wa sekta hiyo kuhakikisha wanasimamia vyema shughuli za uvuvi nchini.



**Pichani wavuvi wakiendelea na shughuli ya uvuvi wa Samaki baharini**

# SERIKALI YATUMIA SH. MILIONI 900 KUKARABATI MABWAWA MAWILI YA KUNYWESHEA MIFUGO

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel amesema kuwa serikali inatumia zaidi ya shilingi Milioni 900 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa Mabwawa mawili ya kunyweshea mifugo ya Narakauo lililopo Wilayani Simanjiro, Mkoani Manyara na Bwawa la Kimokuwa lililopo Wilayani Longido, Mkoani Arusha.

Prof. Gabriel alieleza hayo alipokuwa katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa mabwawa hayo katika Mikoa ya Arusha na Manyara Novemba 7, 2020.

Akiongea na Wafugaji wa maeneo hayo baada ya kufanya ziara hiyo, Prof. Gabriel alisema kuwa bwawa la Narakauo limetengewa milioni 413 wakati bwawa la Kimokuwa limetengewa milioni 511.9.

Prof. Gabriel alieleza kuwa ukarabati huo ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Magufuli alipokuwa Mkoani Manyara hivi karibuni ya kuhakikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi inafanya jitihada za dhati kutatua changamoto ya maji kwa mifugo.

Aliongeza kuwa, mbali na ukarabati wa mabwawa hayo mawili, miradi kama hii ya ukarabati wa mabwawa ya kunyweshea mifugo unaendelea pia katika Kata ya Chamakweza, Chalinze, Mkoani Pwani na mwingine wa Kata ya Mbangala, Mkoani Songwe upo katika hatua za kukamilika, huku akisisitiza kuwa Wizara itaendelea kuboresha upatikanaji wa maji kwa mifugo ili wafugaji waondokane na kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

Aidha, Prof. Gabriel alitumia nafasi hiyo pia kuitaka kampuni ya Ujenzi ya Zeco ambayo ndio imepewa jukumu la kukarabati mabwawa hayo mawili ya Narakauo na Kimokuwa kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika kabla ya Novemba 25, 2020 ili kukwepa changamoto ya mvua.

“Ongezeni nguvu na spidi ya ujenzi huu ili muukamilishe kabla ya mvua hazijaanza, mvua zikiwakuta kabla hamjamaliza, kazi yote mliyoifanya itakuwa haina maana”, alisisitiza Prof. Gabriel



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati) akitoa maelekezo kwa Mhandisi wa Kampuni ya Ujenzi ya Zeco, Gerald Oswald (kulia) alipofanya ziara ya kukagua ukarabati mkubwa wa bwawa la kunyweshea mifugo la Narakauo lililopo Wilayani Simanjiro, Mkoani Manyara Novemba 7, 2020.**

“Tunategemea ujenzi wa mabwawa haya uishe kwa wakati ili yaweze kusaidia wafugaji wetu ,mabwawa haya yatawapunguzia wafugaji kutembea umbali mrefu kutafuta maji”, aliongeza Prof. Gabriel

Akizungumzia bwawa hilo, Mfugaji, kijiji cha Narakauo, Petro Narotoka aliishukuru serikali kwa kutoa pesa hizo kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo huku akiongeza kuwa mradi huo ukikamilika utakuwa ni msaada mkubwa kwa mifugo na jamii kwa ujumla.

“Ujenzi huu ukikamilika tutajitahidi sisi kama wafugaji kulinda miundo mbinu ya bwawa hili ili idumu kwa muda mrefu kwa faida ya jamii yetu”, alisema Narokota

Naye, Mfugaji wa kijiji cha Kimokuwa, Wilayani Longido, Mkoani Arusha, Kasaine Lamaiba alisema kuwa uamuzi huo wa serikali wa kujenga bwawa katika kijiji hicho umeonesha ni kwa kiasi gani serikali inathamini wafugaji nchini.

“Ujenzi wa bwawa hili utasaidia pia visima vya asili vilivyopo hapa kijijini kutumika kwa muda mrefu bila kukauka kwa sababu uwepo wa bwawa hili utaongeza chanzo cha uhakika cha maji”, alisema Lamaiba

Aidha, prof. Gabriel aliuomba uongozi wa Halmashauri za Wilaya hizo za Longido na Simanjiro kuendelea kutoa ushirikiano ili miradi hiyo iweze kukamilika kwa wakati huku akiwaomba kuendelea kuwaandaa jamii kutunza miradi hiyo pindi itakapokamilika.



**Diwani wa Kata ya Demosileti, kijiji cha Narakauo, Wilayani Simanjiro, Mkoani Arusha, Ezekiel Senga (wa pili kulia) akimueleza jambo Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi(mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (kushoto) alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa bwawa la kunyweshea mifugo la Narakauo lililopo Wilayani Simanjiro Mkoani Manyara Novemba 7, 2020.**



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi(mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel(kulia) akiongea na Wafugaji wa kijiji cha Narakauo, Wilayani Simanjiro, Mkoani Manyara alipokuwa njiani kuelekea Mkoani Arusha muda mfupi baada ya kukagua ukarabati wa bwawa la kunyweshea mifugo la Narakauo Novemba 7, 2020.**




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel akiendesha moja ya mitambo inayotumika katika ujenzi wa bwawa la Kimokuwa lililopo Wilayani Longido Mkoani Arusha alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa bwawa hilo Novemba 7, 2020.**



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati waliosimama) akiwa katika picha ya pamoja na Wafugaji na Viongozi wa Kampuni ya ujenzi ya Zeco alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa bwawa la Kimokuwa lililopo Wilayani Longido, Mkoani Arusha Novemba 7, 2020.**

# UTAYARI WA WAFUGAJI KUSHIRIKISHWA KWENYE MIRADI, HUFANYA MIRADI HIYO KUDUMU

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugp na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel amesema wafugaji wanaposhirikishwa katika uchangiaji wa miradi mbalimbali kwa ajili ya mifugo yao wamekuwa wakionyesha utayari na kufanya miradi hiyo kudumu kwa kuwa wanajisikia kuwa sehemu miundombinu hiyo.


Akizungumza (30.11.2020) katika bwawa la kunyweshea mifugo maji la Elwaniolera lililopo kijiji cha Eluwai, Kata ya Monduli Juu, Wilaya ya Monduli Mkoani Arusha, Prof. Gabriel alisema wakazi katika eneo hilo wameonesha utayari wa kulifanyia ukarabati bwawa hilo linalohudumia zaidi ya wafugaji 2,000 katika vijiji vya Eluwai, Emairete na Enguiki kutokana na kina cha bwawa hilo kupungua kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwemo ya kilimo.

"Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli umenieleza kuwa wakazi wa Kata ya Monduli Juu wako tayari kushiriki kwa kiwango kikubwa katika kulifanyia maboresho bwawa hili, wafugaji wanaposhirikishwa nao wako tayari kushiriki na faida yake kubwa hakutakuwa na haja ya serikali kugharamia kila kitu lakini pia wanaposhirikishwa mara zote miundombinu hiyo huwa inadumu kwa kuwa nao watajisikia sehemu ya miundombinu hiyo." Amesema Prof. Gabriel

Aliongeza kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo tayari kulikarabati Bwawa la Elwaniolera kwa kujenga mabirika kwa ajili ya mifugo kunywea maji kwa kuwa hali ilivyo sasa ni hatari kwa mifugo, wachungaji pamoja na usalama wa bwawa lenyewe.

Aidha, Prof. Gabriel alisema wizara itaangalia namna ya kuboresha masuala ya majosho katika vijiji vya Eluwai, Emairete na Enguiki ili kuhakikisha kwamba dhana nzima ya kuboresha afya ya mifugo inafanikiwa.

Pia, alisema wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akizindua



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel akisaini kitabu cha wageni cha Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Mkoani Arusha akiwa katika eneo lililopo Bwawa la Elwaniolera kabla ya kutembea bwawa hilo linalohudumia zaidi ya wafugaji 2,000 kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao maji katika vijiji vya Eluwai, Emairete na Enguiki vilivyopo Kata ya Monduli Juu.**

Bunge la 12 alifafanua kuwa angependa kuona Sekta ya Mifugo inachangia zaidi katika uchumi.


Alibainisha kuwa kwa sasa Sekta ya Mifugo inachangia kwa asilimia 7.64 na inakuwa kwa asilimia tano ambapo lengo la wizara ni kuhakikisha sekta hiyo ifikie kuchangia kwa zaidi ya asilimia 15.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel amesema Kata ya Monduli Juu ina mifugo mingi hivyo masuala ya malisho na afya ya mnyama ni muhimu kwa kuwa na mifugo mingi na bora ni muhimu kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ili wafugaji waweze kunufaika kupitia Bwawa la Elwaniolera ili maji yake yaweze pia kutumika katika shughuli nyingine za kilimo cha umwagiliaji.

Kwa upande wake Afisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli Dkt. Yandru Marmo amemueleza Prof. Gabriel kuwa Bwawa la Elwaniolera limeanza kupungua kina chake kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea katika chanzo cha maji ya bwawa hilo, hali inayosababisha udongo kusafirishwa hadi kwenye bwawa na kusababisha kina chake kuzidi kupungua na kuhofia madhara makubwa kwa wafugaji wanaolitegemea kunyweshea mifugo maji.

Dkt. Marmo aliongeza kuwa ni muhimu kwa bwawa hilo kufanyiwa ukarabati kwa kuwepo kwa mabirika ya kunyweshea mifugo maji ili mifugo isiingie ndani ya bwawa kwa kuwa inachangia pia udongo kuingia ndani ya bwawa pamoja na shughuli za kibinadamu ikiwemo ya kilimo zisifanywe karibu na chanzo cha maji ya bwawa hilo ili kuzuia pia udongo kusafirishwa hadi kwenye bwawa na kusababisha kina chake kupungua.

Bwawa la Elwaniolera lililopo Kata ya Monduli Juu, Wilaya ya Monduli Mkoani Arusha, lilijengwa mwishoni mwa miaka ya 1970 kwa jitihada za serikali wakati Hayati Edward Moringe Sokoine akiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**Muonekano wa Bwawa la Elwaniolera lililopo Kata ya Monduli Juu, Wilaya ya Monduli, Mkoani Arusha ambalo linakabiliwa na changamoto ya kupungua kwa kina chake kutokana na kujaa udongo unaosababishwa na mifugo kunywea maji ndani ya bwawa pamoja na chanzo cha maji ya bwawa hilo kusafirisha udongo hadi kwenye bwawa kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwemo ya kilimo zinazofanywa katika chanzo hicho**

# WATUMISHI WATAKIWA KULITUNZA BASI JIPYA LA WIZARA

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel amewataka Watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha wanalitunza Basi jipya lililonunuliwa kwa ajili ya usafiri wa Watumishi ili liweze kusaidia kuongeza ufanisi wa kazi za Wizara.

Prof. Gabriel aliyasema hayo alipokuwa akikabidhiwa basi hilo aina ya TATA lilipowasili katika Mji wa Serikali, Mtumba, jijini Dodoma Novemba 16, 2020.

Akiongea wakati wa kupokea basi hilo, Prof. Gabriel aliwashukuru Watumishi wa Wizara hiyo kwa uvumilivu wao katika kipindi chote ambapo hapakuwa na usafiri wa uhakika wa kwenda na kurudi kazini huku akisema kuwa basi hilo litatumiwa na watumishi wa sekta zote mbili za Mifugo na Uvuvi.

"Kupata ni jambo moja, lakini kutunza ni jambo lingine, ni lazima kulitunza Basi hili ili litutunze, Basi hili limenunuliwa kwa gharama kubwa, karibu shilingi Milioni 165 hivyo ni muhimu sana kulitunza," alisema Prof. Gabriel

Prof. Gabriel alitumia nafasi hiyo pia kuishukuru Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Idara ya Ununuzi na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kwa uratibu mzuri na kulipendezesha basi hilo.

Aidha, pamoja na mambo mengine, Prof. Gabriel aliitaka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu kuhakikisha inasimamia vizuri suala la ratiba ya Basi hilo ya kupeleka watumishi kazini na kurudi, huku akisema ni muhimu ratiba hiyo ikazingatiwa ili basi lisiwe linasubiri mtu.

Aliongeza kuwa atafurahi kama katika basi hilo wataajiriwa Kondakta na Dereva Wanawake kwani kwa kufanya hivyo sekta hiyo itakuwa ya mfano na itakuwa imeunga mkono kauli ya Rais, Dkt. John




**Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu (Mifugo), Bw. Fraksed Mushi akimkabidhi funguo wa basi jipya kwa ajili ya usafiri wa watumishi aina ya TATA Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel katika eneo la Mji wa Serikali – Mtumba tarehe 16.11.2020**




**Hili ndilo basi jipya la watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.**

Pombe Joseph Magufuli kuhusu wanawake kupewa nafasi.

"Tuajiri Dereva na Kondakta wote wawe wanawake, kina mama wanaweza, tukifanya hivyo tutakuwa sekta ya mfano kwa sababu Rais alipokuwa anazindua Bunge alisisitiza hilo, hivyo ningetamani tuwe sekta ya mfano na ninaamini litawezekana," alisema Prof. Gabriel

Kuhusu utunzaji wa Basi hilo, Prof. Gabriel alitoa maelekezo kwa Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Fraksed Mushi kuhakikisha gari hilo linafanyiwa matengenezo vizuri ya mara kwa mara ili liweze kudumu huku akiongeza kuwa madereva na kondakta wa gari hilo ni lazima wapatiwe mavazi mazuri ili kuboresha muonekano wao.

Naye, Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Fraksed Mushi alimshukuru Katibu Mkuu huyo kwa jitihada alizozifanya mpaka kupatikana kwa Basi hilo na aliahidi kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi kuwa watalitunza Basi hilo ili liweze kuleta tija iliyokusudiwa.

"Tutalitendea haki, Watumishi wamefurahi kwa kutatuliwa hii changamoto ya muda mrefu ya usafiri, ni maamuzi magumu lakini yatakuwa na tija kwenye Wizara, tutalitunza vyema basi hili…," alisema Mushi

Kwa upande wa Watumishi, baadhi yao hawakusita kuonesha furaha yao baada ya kupatikana kwa basi hilo huku wakisema kuwa ujio wa basi hilo umejibu changamoto yao ya muda mrefu kuhusu usafiri.

Msaidizi wa Ofisi ya Utawala na Rasilimali Watu, Moses Kabeho alimshukuru Katibu Mkuu kwa jitihada zake mpaka kufanikisha kutatua kero hiyo ya usafiri huku akisema kuwa Basi hilo litawasaidia kufika kazini kwa wakati.

"Tunamshukuru Katibu Mkuu pamoja na Uongozi wa Wizara kutatua changamoto ya usafiri kwani sasa kwa ujio wa Basi hili itaturahisishia utendaji wetu wa kazi," alisema Kabeho

Naye, Msaidizi wa Kumbukumbu Mwandamizi, Grace Ngowi alimshukuru Katibu Mkuu na Menejimenti kwa ujumla kwa kuwaletea usafiri huo kwani utasaidia kuongeza ufanisi wa kazi.

# MRADI WA SWIOFish WASHIRIKISHA WANANCHI KULINDA RASILIMALI ZA UVUVI NCHINI

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah amesema Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi Mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) umewezesha uboreshaji wa miundombinu ya taasisi za wizara hiyo katika kuhakikisha serikali kwa kushirikiana na wananchi inalinda rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam Novemba 20, 2020 akiwa na lengo la kuwafahamisha manufaa ya mradi wa SWIOFish, Dkt Tamatamah alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umewanufaisha pia wavuvi wa Pwani ya Bahari ya hindi, wakulima wa Mwani, wafugaji wa viumbe maji na wachakataji wa mazao ya uvuvi wakiwemo wanawake na jamii inayozunguka maeneo hayo.

"Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kimataifa na malengo mengine ni kujenga uwezo wa nchi katika kusimamia rasilimali za uvuvi, kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa Bahari kuu, kuinua uchumi wa jamii ya watu wa Pwani na kuinua pato la taifa kutokana na rasilimali za uvuvi. Amesema Dkt. Tamatamah

Aidha, Dkt. Tamatamah alisema tangu mradi huo uingie hapa nchini Mwezi Juni Mwaka 2015 ambapo unatarajia kukamilika Mwezi Septemba Mwaka 2021 uvuvi haramu wa kutumia baruti na mabomu umedhibitiwa kwa asilimia 100 kutokana na kuimarishwa kwa doria pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa jamii ya Pwani kuhusu madhara ya uvuvi haramu.

Pia, alisema usajili wa vyombo vya uvuvi umeongezeka hadi kufikia asilimia 58 kutoka asilimia 25 ya awali kabla ya mradi kutokana na usimamizi wa utekelezwaji wa sheria na kanuni za uvuvi, umewezesha tafiti mbalimbali ambapo matokeo yake yametumika kurekebisha baadhi ya kanuni za uvuvi ambazo zimesaidia kuongezeka kwa samaki wanaovuliwa pamoja na kuongezeka kwa uvuvi wa karibu wa kutumia ndoano kwa maeneo mengi.

"Mafanikio mengine ya Mradi wa SWIOFish ni pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na uvuvi hususan kwenye halmashauri ambapo Halmashauri ya Pangani yameongezeka kutoka milioni 55 mwaka 2016/17 hadi kufikia Milioni 235 mwaka 2018/19." alibainisha Dkt. Tamatamah




**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah akiongea na Waandishi wa habari (hawapo pichani) baada ya kufungua kikao cha Sekta ya Uvuvi na wahariri wa vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya mradio huo. Kikao kimefanyika katika ofisi ndogo za wizara hiyo jijini Dar es Salaam tarehe 20.11.2020.**

Katika kikao hicho na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah alitumia muda huo kuelezea pia namna mradi wa SWIOFish ulivyoimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kufadhili mafunzo ya uvuvi endelevu ambayo yamesaidia baadhi ya wavuvi kutekeleza kwa hiari usimamizi wa rasilimali za bahari.

Aliongeza kuwa mradi umeanzisha vikundi hamsini vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika Wilaya tano za mfano na kuimarisha utunzaji wa mazingira ya Pwani, viwango vya dagaa pamoja na Mwani vimeandaliwa na kupitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Katibu mkuu huyo pia alisema mradi umewezesha ujenzi wa maabara ya utafiti iliyoko Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) jijini Dar es Salaaam, ujenzi wa nyumba tatu za watumishi wa Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), kituo cha Tanga Silikanti kilichopo Kigombe, wilayani Muheza, na ujenzi wa ofisi tano za BMU katika Wilaya za Mkinga (Zingibari), Pangani (Kipumbwi), Chalinze (Saadani), Bagamoyo (Dunda) na Lindi vijijini (Sudi).

Kwa upande wake Mratibu wa mradi wa SWIOFish Tanzania Bara Bw. Nichrous Mlalila alisema licha ya mafanikio ya mradi changamoto mbalimbali zimekuwa zikijitokeza zikiwemo za ugumuwa uoatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za kila siku za BMU, kutokea kwa baadhi ya maeneo ya uvuvi haramu wa kutumia nyavu zisizofaa kisheria na upatikanaji wa takwimu sahihi katika mifumo ya ukusanyaji taarifa.

Bw. Mlalila alisema hadi sasa asilimia 65 ya shughuli za mradi zimetekelezwa na kukamilika, ambapo asilimia nane (8) zipo katika utekelezaji kwa zaidi ya asilimia 75, asilimai 19 ya shughuli za mradi zinaendelea kutekelezwa kati ya asilimia 25 hadi 75 ya utekelezaji. Asilimia nne (4) zipo katika utekelezaji wa asilimia chini ya 25. Aliongeza kuwa unaonyesha matokeo chanya na upo katika mwelekeo mzuri wa utekelezaji.

Akizungumza kwa niaba ya wahariri wa vyombo vya habari waliohudhuria kikao hicho Kaimu Mhariri Mkuu wa gazeti la Habari Leo Bw. Mgaya Kingoba ameishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi Sekta ya Uvuvi kwa kuendelea kuwapatia taarifa mbalimbali na elimu juu ya sekta hiyo ambazo zinawasaidia kutoa taarifa sahihi kwa umma.

Pia, amewaomba wahariri wenzake kuendelea kuinga mkono wizara hiyo katika kuhakikisha inatoa taarifa ambazo zitasaidia kulinda rasilimali za uvuvi pamoja na kupambana na uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mradi wa SWIOFish unatekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA) na Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) katika maeneo ya Pwani ya Tanzania katika wilaya tano za mfano zikiwemo Mkinga, Tanga Jiji, Pangani, Bagamoyo na Lindi Vijijini. Kwa upande wa Zanzibar, Mradi unatekelezwa na Wizara ya Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi pamoja na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA).



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah (aliyekaa katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wahariri wa vyombo vya habari nchini, na baadhi ya maafisa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya mradi wa SWIOFish, baada ya kufungua kikao cha Sekta ya Uvuvi na wahariri wa vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya mradio huo. Kikao kimefanyika katika ofisi ndogo za wizara hiyo jijini Dar es Salaam. (20.11.2020)**



Jarida hili la Mtandaoni hutolewa kila mwezi na

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
**Wizara ya Mifugo na Uvuvi,**
S.L.P. 40487, Dodoma,Tanzania
Simu: +255763 255255
Email: www.mifugouvuvi.go.tz
Tovuti: www.mifugo.go.tz